"Tunayaangaza maisha yako"

**TANESCO MAKAO MAKUU, S.L.P. 453, DODOMA, TANZANIA, SIMU 180**

**TAARIFA KWA WATOA HUDUMA WA TANESCO**

**Jumatatu, Oktoba 06, 2025**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linaendelea na zoezi la kuboresha mifumo ya huduma za malipo na kuhuisha taarifa za watoa huduma wote wanaofanya kazi na TANESCO kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Kwa kuzingatia hilo, TANESCO inawaomba watoa huduma wote wanaofanya biashara na Shirika kuwasilisha taarifa zifuatazo mapema iwezekanavyo:

i. Jina la Kampuni au Biashara
ii. Mwaka wa Kuanzishwa Biashara
iii. Anuani ya Biashara
iv. Namba ya Simu ya Biashara
v. Anwani ya Barua Pepe ya Meneja Fedha na Mhasibu anayefuatilia madeni
vi. TIN Namba na VRN Namba ya Kampuni
vii. Jina la Benki, Namba ya Akaunti, Bank IBAN, Swift Code, na Sarafu ya Malipo (Currency of Payment)
viii. Bidhaa au Huduma Inayotolewa
ix. Uzoefu katika kutoa huduma kwa TANESCO (ikiwa umewahi kutoa, tafadhali taja tawi husika na anuani yake)

Taarifa hizo ziwasilishwe kupitia barua pepe: devitha.nyakunga@tanesco.co.tz

Mwisho wa kuwasilisha taarifa hizi ni tarehe **30 Oktoba 2025**, ili kuepusha usumbufu wowote upande wa malipo, hakikisha taarifa zako zinawasilishwa kwa wakati.

Tunawashukuru kwa ushirikiano wenu.

Imetolewa Na:

**KURUGENZI YA MAWASILIANO NA HUDUMA KWA WATEJA TANESCO**
**MAKAO MAKUU**
**DODOMA**